# SURUA (MEASLES)

## SI TU VIPELE VIDOGO



### Ugonjwa wa surua unaweza kuwa hatari, hasa kwa watoto wachanga na watoto wadogo.

### Dalili za ugonjwa wa surua kwa kawaida zinajumuisha:

- **Joto jingi mwilini** (unaweza kuongeza joto mwilini hadi zaidi ya 104°F)
- **Kikohozi**
- **Kumwaga kamasi**
- **Macho mekundu na/au yanayomwaga machozi**
- **Vipele** (hulipuka siku 3 hadi 5 baada ya dalili kuanza)

## Ugonjwa wa surua unaweza kuwa hatari.

Ugonjwa wa surua unaweza kusababisha matatizo makubwa ya afya, ikijumuisha ugonjwa wa nimonia, kuvimba ubongo (encephalitis) na kifo.

**Mtu 1 kati ya watu 5** wanaoambukizwa ugonjwa wa surua hulazwa hospitalini.

**Mtoto 1 kati ya watoto 20** wenye ugonjwa wa surua hupata ugonjwa wa nimonia, ambao ni sababu ya kawaida zaidi ya kufa kutokana na ugonjwa wa surua kwa watoto wadogo.

**Mtu 1 kati ya watu 1,000** wenye ugonjwa wa surua huvimba ubongo, hali ambayo inaweza kusababisha uharibifu wa ubongo.

**Mtu 1 hadi 3 kati ya watu 1,000** wenye ugonjwa wa surua hufa.

**Ugonjwa wa surua unaambukiza sana** na huenezwa kupitia hewani wakati mtu aliyeambukizwa anakohoa au kupiga chafya. Mtu mmoja mwenye ugonjwa wa surua anaweza kuueneza kwa watu 9 kati ya 10 ambao hawajachanjwa walio karibu naye.



## Chanjo ni njia bora zaidi ya kuzuia ugonjwa wa surua

Mtoto anapaswa kupata chanjo ya surua-matumbwitumbwi-rubela (Measles-Mumps-Rubella, MMR) akiwa na umri wa miezi 12 hadi 15 na miaka 4 hadi 6. Dozi mbili huzuia ugonjwa wa surua kwa kiwango cha 97%.

Chanjo kwa Watoto
Iowa HHS

Chanjo kwa Watu Wazima
Iowa HHS

IOWA MEDICAL SOCIETY

Original content created by CDPH